# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR NA KUWEKA MASHARTI YANAYOHUSIKA NA HUDUMA ZA MIUNDOMBINU YA TEHAMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.

UTANGULIZI:

**Mheshimiwa Spika,**

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine tena tukiwa hai na wazima wa afya ambayo ni neema kubwa kwetu kwani wengine hawakujaaliwa kuipata.

**Mheshimiwa Spika,**

Pili napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuona haja ya kuja na Mswada huu ambao ni muhimu kwa maendeleo ya kukuza Teknolojia ya Mawasiliano Zanzibar ambao utakuja kuondosha changamoto mbali mbali ziliopo sasa.



Edit with WPS Office

**Mheshimiwa Spika,**

Pia,shukrani za dhati ziwaendee wadau wote walioshiriki katika kutoa maoni mbali mbali yenye tija kwa mswada huu ambayo yameiwezesha kamati yetu kuweza kuupitia na hatimae leo hii kuja na maoni ambayo tunaamini yatasaidia sana kuweza kufikiwa lengo lililokusudiwa katika kuanzisha **"Shirika la Mawasiliano Zanzibar"** lenye kuleta tija na kupiga hatua katika suala zima la kuikuza Teknolojia ya Mawasiliano kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile pongezi za pekee ziende kwa wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanayofanya na ushirikiano wanaouonesha kwa pamoja wakati walipokua wakipitia Mswada huu kuanzia kwa Wadau hadi kukaa na Wizara na kuweza kutoa maoni yao leo hii, naomba sasa niwatambue wajumbe wanaounda kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Yahya Rashid Abdallah — Mwenyekiti
2. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Mussa Foum Mussa — Mjumbe
4. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu — Mjumbe
5. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe — Mjumbe
6. Mhe. Bahati Khamis Kombo — Mjumbe

Aidha, Kamati hii ina makatibu wawili ambao wanaiwezesha kutekeleza majukumu yake kitaalamu na kiufanisi zaidi. Makatibu hao ni :-

1. Ndg. Rahma Kombo Mgeni, na
2. Ndg. Himid Haji Choko



Edit with WPS Office

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo naomba sasa kutoa maoni ya kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilikaa na wadau mbali mbali kwa mujibu wa kanuni ya 84(8) toleo la 2020 kwa lengo la kupokea maoni kuhusiana na Mswada huu na kuweza kuisaidia Kamati wakati wa kuupitia na kuuchambua mswada ili kuweza kuja na mapendekezo ambayo yataweza kusaidia kupatikana kwa Sheria nzuri na yenye kutekelezeka kwa manufaa ya maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kupitia kwa kina Mswada huu kamati imeweza kurekebisha baadhi ya vifungu vilivyomo kweye Mswada huu kwa kufuta na kuandika upya, kurekebisha baadhi ya maneno ili kuweza kusomeka vizuri na kuleta maana na kuweka sawa lugha, na kuongezwa kwa baadhi ya vifungu vipya ili kuleta mtiririko mzuri wenye kuleta maana katika Mswada huu, baadhi ya vifungu hivyo ni kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 3 kinarekebishwa katika tafsiri ya maneno yafuatayo:-

(a) Kuwepo kwa ufafanuzi wa tafsiri ya neno **"TEHAMA"** kama ifuatavyo:

**'TEHAMA" maana yake ni teknolo**

**jia zinazotumika katika kukusanya, kuhifadhi au kutuma taarifa na zinajumuisha zile zinazohusisha matumizi ya kompyuta au mfumo wowote wa mawasiliano".**



Edit with WPS Office

(b) Kuongezwa kwa tafsiri mpya ya neno **"Miundombinu ya Kimkakati ya TEHAMA"** maana yake ni **"miundombinu ya TEHAMA inajumuisha Kituo Kikuu cha Taifa cha Kuhifadhi Taarifa, Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano pamoja na miundombinu mengine itakayoamuliwa na Waziri".**

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 7 kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) Kufutwa aya ya (c).

(b) Kufutwa aya ya (d) na kuandikwa aya ya (d) mpya kama ifuatavyo:

**"(d) kusajili anuani mtandao (vikoa) ndani ya Zanzibar kwa Serikali na Taasisi au Kampuni binafsi."**

(c) Kufutwa aya ya (e).

(d) Kufutwa aya ya (f) na kuandikwa aya ya (f) mpya kama ifuatavyo:

**"(f) kutoa miongozo ya matumizi ya miundombinu ya kimkakati ya TEHAMA inayomikiliwa na Shirika."**

(e) Kufutwa aya ya (h) na kuandikwa aya ya (h) mpya kama ifuatavyo:

**"(h) kutoa ruhusa ya matumizi na uunganishwaji wa miundombinu ya kimkakati ya TEHAMA inayomilikiwa ya Shirika."**

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo la marekebisho haya ni kuliwezesha Shirika kuwa na nguvu ya kutoa ruhusa ya matumizi na uunganishwaji wa miundombinu ya TEHAMA ili kuweza kuzuia utumiaji holela wa miundombinu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile katika Kifungu cha 26 kinarekebishwa kama ifuatavyo:



Edit with WPS Office

(a) katika kifungu kidogo cha (2), kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

**"(2) Shirika litakuwa chombo pekee kinachoruhusiwa kujenga miundombinu ya kimkakati ndani ya Zanzibar."**

(b) katika kifungu kidogo cha (3), kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

**"(3) Bila kuathiri masharti ya Kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Shirika linaweza kushirikiana na wawekezaji au Sekta binafsi yoyote katika ujenzi na usimamizi wa miundombinu ya kimkakati ya TEHAMA."**

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo la marekebisho haya ni kutoa fursa kwa wawekezaji wa sekta binafsi kuweza kushirikiana na Shirika katika ujenzi na usimamizi wa miundombinu ya kimkakati ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,**

Marekebisho yote yaliyofanywa na Kamati yanapatikana katika karatasi ya marekebisho iliyomo kwenye vishkwambi vyetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi na kuunga mkono uamuzi wa kuanzishwa Shirika la Mawasiliano ambalo litasaidia kuleta mabadiliko ya haraka ya TEHAMA ambayo kwa kiasi kikubwa yatachangia katika ukuaji wa uchumi. Kamati imejuilishwa kuwa kuanzishwa kwa Shirika la Mawasiliano kutaweza kuondosha changamoto mbali mbali ziliopo sasa ikiwemo :-



Edit with WPS Office

- Kushindwa kutekeleza miradi ya maendeleo ya Taasisi kutokana na utegemezi wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kitu ambacho kinakwaza katika utekelezaji wa kazi kwa wakati.
- Uwepo wa changamoto za kimuundo ambazo hazitoi fursa kwa Wakala kufanya Maamuzi
- Sheria iliyopo haitoi fursa za uwekezaji kwenye masuala ya huduma na miundombinu ya mawasiliano
- Vile vile Sheria iliyopo haisaidii katika kudhibiti udukuzi na ujasusi wa kimitandao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati kwa mara nyengine tena inakubaliana na dhamira ya kuanzishwa kwa Shirika la Mawasiliano hasa katika masuala ya udhibiti wa udukuzi wa mitandao ambapo kwa sasa imekua ni changamoto kubwa kote ulimwenguni na kupelekea athari hasa katika masuala ya usalama wa nchi. Hivyo kamati inasisitiza iwapo Serikali imeamua kuanzisha Shirika hili basi ichukue jitihada na tahadhari za hali ya juu katika kuhakikisha inadhibiti vizuri masuala yote yatokanayo na udukuzi na ujasusi ili kuiweka salama nchi yetu katika masuala mazima ya Mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati itafarajika iwapo dhamira njema hii itatekelezwa kwa vitendo na kuleta ile tija iliyokusudiwa kwa Serikali ambayo itawezesha kutoa fursa za uwekezaji kwenye masuala ya huduma na miundombinu ya mawasiliano pamoja na Zanzibar kuweza kujitangaza kwenye “Cyber Space “.


Edit with WPS Office

**Mheshimiwa Spika**

Lakini pia, tunaendelea kusisitiza jitihada zichukuliwe katika kuhakikisha Shirika linaendeshwa kwa ufanisi wa hali ya juu ili huduma zilizokusudiwa kupatikana kwa kiwango kizuri na kuwepo kwa wataalamu wenye ujuzi wa kuendesha Shirika katika nyanja zinazohitajika na uwepo wa miundombinu ya kisasa ambayo itawezesha kupatikana huduma kwa kiwango cha juu.

**Mhehimiwa Spika,**

Kamati inatoa wito kwa wizara kuhakikisha Shirika linaendeshwe kitaalamu na kupatikana huduma kama ilivyokusudiwa na kuachana na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea ambapo mwisho wa siku kunapelekea hasara kwa Serikali na Shirika kushindwa kujiendesha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatarajia malengo yaliyokusudiwa katika kuanzishwa kwa Shirika hili iwapo yatafikiwa basi yataweza kuleta mabadiliko makubwa hasa katika huduma za mawasiliano na kuondosha changamoto ziliopo sasa ambazo zinakwaza katika kupiga hatua za maendeleo katika masuala mazima ya **TEHAMA.**

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maoni hayo, naomba kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii kutoa maoni ya Kmati yangu mbele ya Baraza lako, na nawaomba Wajumbe wa Baraza lako wauchangie Mswada huu na kutoa maoni na mapendekezo yao kwa madhumuni ya kuboresha na hatimae kuupitisha na baadae kuwa sheria kama ilivyokusudiwa.



Edit with WPS Office

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

………………..

**Mhe Yahya Rashid Abdallah**

Mwenyekiti,
Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,
Baraza la Wawakilishi
**Zanzibar.**



Edit with WPS Office